HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

TAARIFA FUPI YA UTEKELEZAJI WA KAZI YA URASIMISHAJI WA ARDHI KATIKA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

MKURABITA ni neno ambalo limezoeleka sana hapa Njombe kwa sasa mpaka imefikia wakati mtu uchumi ukiyumba kidogo wanasema ***"ah jamaa hana MKURABITA"*** Lakini tafsiri halisi ni Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania na ulianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na unasimamiwa na Ofisi ya Rais – Ikulu.

Tathmini ya Urasimishaji ilianza kwa mara ya kwanza mwaka 2008 baada ya Mkurugenzi wa uendeshaji – MKURABITA kufika katika Halmashauri yetu na kujionea mwenyewe jinsi wananchi wa Njombe wanavyothamini na kuitumia Ardhi yao kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kutokana na Ardhi ya Wananchi wengi wa Njombe kutokuwa rasmi na Wananchi wengi wa Njombe kujishughulisha kikamilifu na shughuli mbalimbali za kiuchumi hususani Kilimo na Biashara, Ofisi ya Rais Kitengo cha MKURABITA kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Njombe

tuliamua kurasimisha Ardhi katika Vijiji nane vya Halmamashauri ya Mji Njombe na kuanza utekelezaji katika Kijiji cha Kifanya Kata ya Kifanya.

Mbali na Urasimishaji Vijiji, mnamo mwezi Oktoba 2009, MKURABITA kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Njombe tulianza Urasimishaji Ardhi katika Mji wetu kwenye Mitaa ya Melinze, Joshoni na Mpechi iliyoko Kata ya Njombe Mjini.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika utekelezaji wa kazi hii, wananchi walionyesha mwitikio wa hali ya juu, kwani walihudhuria katika vikao vyote shirikishi na walifika ofisini pale tulipowataka wafike kuleta baadhi ya taarifa na kusaini nyaraka zao. Hali iliyofanya utekelezaji wa urasimishaji Ardhi kuwa rahisi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Lengo kuu la Mpango huu ni kuweka mfumo Rasmi wa Umiliki wa Rasilimali Ardhi ili wamiliki wa asili wa Ardhi waweze kutambulika kisheria na kuwa na Anuani za Ardhi zao. Limechukuliwa eneo dogo la mfano lakini nia hasa ya MKURABITA ni kuijengea uwezo Halmashauri ili iweze kuendelea kurasimisha katika maeneo mengine yaliyobaki.

Kazi zilizofanyika katika eneo la Mpango wa Urasimishaji Ardhi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika eneo hilo la urasimishaji kazi zilizofanyika ni utambuzi wa wamiliki wa Ardhi na upimaji wa Ardhi ambapo jumla ya viwanja 1,003 vilipimwa kwa gharama ya Tshs 108,027,150/=.

Kati ya viwanja vilivyopimwa, viwanja 597 vimeidhinishwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi viwanja vingine 406 mchakato unaendelea. Jumla ya Rasimu za Hati miliki za Ardhi 314 zimetayarishwa. Hati 106 tayari zimesajiliwa, Hati 137 zipo katika Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Kanda ya Kusini Magharibi - Mbeya kwa ajili ya usajili hati 71 zipo katika hatua za ukamilishwaji katika Ofisi ya Ardhi- Halmashauri ya Mji Njombe.

Aidha wananchi 283 hawajajitokeza kujaza fomu za maombi ya Hati miliki kwa ajili ya maeneo yao.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika mchakato huu wananchi wote waliorasimishiwa Ardhi zao walitakiwa kulipia Tshs 120,000/= tu kwa nyumba ya kuishi, Tshs 200,000/= tu kwa nyumba ya Makazi na Biashara na Tshs 300,000/= tu kwa nyumba za Biashara pekee. Jumla ya wamiliki 281 wamechangia gharama za urasimishaji na jumla ya fedha taslimu Tshs 29,347,000/= zimekusanywa na Halmashauri ya Mji Njombe.

Mafanikio ya Mpango.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

i. Eneo hili lililorasimishwa lilikuwa ni eneo lililojengwa kiholela sasa ujenzi wa aina hii utakoma kwa kuwa kila shughuli inayofanyika juu ya Ardhi inatakiwa kuwa Rasmi.
ii. Wananchi wameukubali na kuupokea Mpango uweze kufanyika katika maeneo yao kwa kuchangia bila kulazimishwa jumla ya Tshs 29,347,000/=.

iii. Kuleta hamasa na hamu ya wananchi kuthamini ardhi yao, tayari wananchi wa Mitaa mingine wameleta barua za maombi ya kutaka kufanyiwa urasimishaji wa Ardhi zao.

iv. Kutatua baadhi ya migogoro ya Mipaka na Migogoro ya Umiliki wa Ardhi katika eneo lililorasimishwa.

Changamoto

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kila jambo linalofanyika linakuwa na changamoto zake, hali kadhalika katika utekelezaji wa Mpango huu, zipo changamoto zilizojitokeza kama ifuatavyo:-

1. Upatikanaji wa taarifa ambazo si sahihi kwa baadhi ya wamiliki wa nyumba na Ardhi.
2. Kuwepo kwa uchangiaji hafifu wa gharama za urasimishaji, jambo linalokwamisha zoezi zima la usajili wa nyaraka za umiliki.
3. Kasi ndogo ya wananchi kufika katika ofisi za Ardhi kutia saini katika nyaraka zinazohusiana na umiliki pia baadhi ya wananchi kuishi nje ya Wilaya ya Njombe.
4. Uvumi kwamba Hati zitolewazo sio halisi kwa kuwa mchakato wa upatikanaji unakwenda haraka.
5. Wananchi 283 kutofika Ofisi za Ardhi kuchukua fomu za maombi ya Hati miliki ya maeneo yao.

Matarajio.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kufuatia zoezi zima lilivyofanywa na ofisi ya Rais – Kitengo cha MKURABITA kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji Njombe,

Halmashauri imepata somo na zaidi sana imepata kianzio (seed capital) hivyo tunatarajia kuendelea na Urasimishaji wa maeneo mengine ambayo bado hayajapimwa. Kwa sasa maeneo yatakayo fanyiwa kazi ni pamoja na Nzengelendete, Matalawe, Mjimwema, Ramadhani, Kihesa na Kibena. Maeneo hayo yameainishwa kufuatia hitaji la wananchi baada ya kujifunza toka kwa majirani zao (yaani mitaa ya Melinze, Mpechi na Joshoni) na kujua faida mkabala baada ya Ardhi kurasimishwa.

Shukrani

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa namna ya pekee tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Ofisi ya Rais – MKURABITA kwa jitihada na ujuzi wa hali ya juu waliowaachia wataalam wa Idara ya Ardhi kwani sasa Halmashauri kwa kutumia wataalam wetu tuna uwezo wa kuendelea kurasimisha Ardhi katika maeneo mengine na kuendelea kuwaletea tija wananchi wetu.

Mwisho tunakushukuru sana **Mheshimiwa Mgeni Rasmi** kwa kukubali kujumuika nasi leo ili kukabidhi Hati Miliki za Ardhi kwa wananchi wa Halmashauri ya Mji Njombe.

Naomba kuwasilisha!